

Cambridge IGCSE™

SWAHILI**0262/02**

Paper 2 Listening

May/June 2026

TRANSCRIPT

Approximately 45 minutes

This document has **8** pages.

Eng: Cambridge International
Cambridge IGCSE Examination in Swahili
Paper 2 Listening, May/June 2026
Turn over now.

(Pause 5 seconds.)

TLR: Zoezi 1

TLR: Utasikia vipande vinane vifupi vilivyorekodiwa.
Jibu swali 1–8 katika nafasi uliyopewa.
Majibu yako yawe mafupi iwezekanavyo.
Utasikia kila rekodi mara mbili.

TLR: Swali 1

M: * Ziada, matembezi yako kwenda ngome kongwe yalikuwaje?

F: Mazuri mno! Najua watu wengi hawapendi lolote zaidi ya kuchunguza mizinga ya zamani iliyopo eneo hilo. Mimi nilifurahi mno kugundua kuwa kulikuwa na vyungu vilivyotumiwa na kumilikiwa na watu walioishi hapo zamani za kale.

M: Kweli wewe ni mtu tofauti na wengine, mimi ninavutiwa na vibanda vya sanaa vinavyouza vitu. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Swali 2

F: * Compton, niambie kuhusu likizo ya krismasi, ulifanya nini?

M: Familia yangu ina desturi ya kupeana zawadi siku ya krismasi. Wazazi wangu walininunulia mtandio mzuri – tena ulikuwa wa rangi ninayoipenda sana. Mwanzo nilitaka kuwapa soksi za krismasi, lakini nikabadili mawazo. Nimeshukuru wamefurahishwa na picha niliyowapa kwani wameibandika ukutani mwao. Nimefarajika kwani niliipiga mimi mwenyewe.

F: Safi sana. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Swali 3

M: * Hadi sasa hatujafikiria shughuli ya kufanya ili kuadhimisha miaka 50 ya ndoa ya bibi na babu. Una mawazo yoyote?

F: Tungeweza kumpa kila mmoja wao zawadi yake. Babu atapenda shati na bibi atafurahia nguo. Lakini labda tule nao?

M: Mwaka uliopita tulipika chakula nyumbani na kula nao. Ninadhani ni bora zaidi kuwachukua mahala kama mgahawani. Sina hamu ya kuenda kwenye nyumba ya michezo ya kuigiza halafu wakalalamika kuwa kuna giza kubwa. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Swali 4

- F:** * Lazima tutazame hali ya hewa itakuwaje kesho kama tunataka kuenda baharini kwa sababu sitaki kufika huko na kukuta mvua inanyesha.
- M:** Ndio. Ninadhani tunaweza kujitandaza juani kesho ingawa kutakuwa na upepo mkali. Kwa mawazo yangu tuende kesho-kutwa ambapo hakutanyesha na pia upepo utakuwa mwanana.
- F:** Upepo ukiwa mkali unaweza kupeperusha vitu vyetu – au hata kutupeperusha sisi wenyewe.
- M:** Ndio hasa! **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Swali 5

- M:** * Tutazame nini leo jioni?
- F:** Kuna programu ya mapishi ambayo nimekuwa nikiisubiri kwa muda. Watu tofauti hualikana majumbani kwao na tunaweza kuona wanachopika.
- M:** Lazima nitalala baada ya dakika chache za kutazama kipindi hicho. Ninapendelea zaidi vipindi vya muziki.
- F:** Hivyo vimezidi kuwa na kelele. Labda tutafute vichekesho ili tutulize akili kidogo.
- M:** Sawa – ingawa sijaona vipindi hivyo vikitangazwa hivi karibuni. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Swali 6

- M:** * Eti Jamilla, mama na baba watafika saa ngapi leo?
- F:** Kusema kweli Juma mimi sina uhakika. Hata hivyo, walisema watapitia soko kuu kununua nyama na mboga. Baba alitaka wanunue hivyo vitoweo kabla ya safari kwa sababu alihofia foleni za magari, lakini mama alihisi vitu vingeoza.
- M:** Wangewahi kufika nyumbani kama wangekuja moja kwa moja. Ningalijua ningaliwashauri wanunue barafu na kuizungushia nyama.
- F:** Kweli. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Swali 7

M: * Hivi kaka yako alikuwa maktabani leo asubuhi?

F: Mara nyingi yeye hupenda kuenda hapo, hasa siku za wikendi. Lakini leo alienda shambani kwetu. Alitoka nyumbani asubuhi hata kabla ya kunywa chai.

M: Basi labda atatuletea mazao mengi atakayovuna huko.

F: Sidhani kama ameweza kufanya hivyo kwani alinipigia simu dakika kumi zilizopita akiniarifu kwamba yupo njiani kurudi nyumbani. Amekimbia manyunyu.

M: Hata mimi sipendi mvua. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Swali 8

F: * Unafanya nini Selemani?

M: Ninajaribu kutengeneza picha ili kumpa baba siku yake ya kustaafu. Nilijaribu kumchora na kutumia rangi zangu kupendzesha taswira yake lakini sikupenda kwa sababu rangi zangu zimeanza kufifia. Sasa nimeamua kuchukua majani ya migomba yaliyokauka na kutengeneza picha ya dau baharini. Ninadhani atafurahia hiyo zaidi. Ningaliweza, ningalichonga ubao lakini sina uwezo huo.

F: Baba yako atafurahia chochote kwani zawadi ni upendo. **

*(Pause 10 seconds. Repeat from * to **. Pause 5 seconds.)*

TLR: Huu ndiyo mwisho wa Zoezi 1. Baada ya muda mfupi utasikia Zoezi 2. Tumia muda huu kusoma maswali ya Zoezi 2.

(Pause 30 seconds.)

TLR: Zoezi 2

TLR: Utamsikia msichana anaongea kuhusu bustani ya mimea.
Msikilize na malizia sentensi.
Andika neno moja au maneno mawili tu katika kila nafasi.
Utasikia rekodi mara mbili.

F: * Mimi ni Rukia na leo ninataka kuzungumza kuhusu bustani ya mimea iliyo jijini kwetu.

Bustani yenyewe ilianzishwa mwaka 1893 na serikali ya kikoloni ya Ujerumani. Sababu kuu ya kuianzisha ilikuwa kupanda mazao ya malighafi kama kahawa ili kuona kama yangestawi pale. Polepole bustani ikageuka na kuwa sehemu ya kujifunza kuhusu mimea na pia kufanyia utafiti. Leo hii lengo kuu la bustani ni kuhifadhi mimea.

Bustani imegawanywa katika maeneo tofauti. Kuna eneo la miti aina ya minazi ambapo kuna mimea kama michikichi. Eneo la matunda kama makomamanga na matufaha. Eneo ninalolipenda mimi ni lile lenye mimea dawa kama miarobaini. Eneo hilo lina kila aina ya miti ingawa mingi hata siujui kwa jina. Nilipokuwa mtoto nilipenda kuja bustanini na rafiki zangu. Tulivutiwa zaidi na eneo lililopandwa mibuyu. Si kwa sababu mibuyu ni miti mikongwe kuliko

yote duniani, ni kwa sababu tuliweza kucheza mchezo wa kujificha hasa kwa vile eneo hilo lilikuwa na majani marefu makavu. Majani hayo yalikatika kirahisi kwa hivyo ilibidi kuwa waangalifu tulipocheza.

Miaka miwili iliyopita nilikuja kufanya matembezi kwenye bustani. Nilifurahi kuona jinsi mimea ilivyozidi kupendeza ingawa nilisikitika kuona kwamba kulikuwa na taka nyingi za plastiki. Pia makorokoro yalikuwa yameenea kote. Nilipata hisia kwamba eneo hilo halikutunzwa vizuri nikaamua kuanza mipango ya kuomba nafasi ya kujitolea. Jambo hili lingeboresha usafi wa bustani. Nilijibiwa papo hapo na tangu wakati huo, bustani imekuwa maarufu kwa wenyeji na wageni. Watu huja kufanya mazoezi ya kukimbia au kutembea huku wakifurahia mandhari. Wengine huja na vyakula vyao na kujitandaza kwenye majani huku wakifurahia pikniki yao ingawa ni muhimu kuwakumbusha kutoacha uchafu majanini. Kwa maoni yangu, ingekuwa afadhali kupiga marufuku kuleta chakula bustanini. Halafu hivi sasa bustani inatoa huduma ya kuwazungusha wageni na kuwafahamisha kuhusu mimea na umuhimu wa kutunza bustani.

Ninahisi uboreshaji umefanya ndege na wanyama wengine wanaoishi hapa kufarijika sana. Idadi ya ndege duniani imeanza kushuka hivyo ndege wanahitaji msaada wetu ili kuepuka athari za uchafuzi wa mazingira. Sisi tumeweza kuwasaidia kujenga viota vyao. Bila shaka inawakera watafiti pale wanapoiba matunda yao, ingawa kwa wageni, ni kelele za ndege zinazowaudhi. **

(Pause 30 seconds.)

TLR: Sasa sikiliza tena.

*(Pause 3 seconds. Repeat from * to **. Pause 30 seconds.)*

TLR: Huu ndiyo mwisho wa Zoezi 2. Baada ya muda mfupi utasikia Zoezi 3. Tumia muda huu kusoma maswali ya Zoezi 3.

(Pause 30 seconds.)

TLR: Zoezi 3

TLR: Utawasikia watu sita wakizungumza kuhusu kuhudhuria onyesho la muziki.

Oanisha wasemaji na mawazo katika orodha A–G.

Kwa kila msemaji, andika herufi (A–G) katika mstari wa jibu.

Tumia kila herufi mara moja tu. Kuna herufi ya ziada isiyohitajika.

Utasikia rekodi mara mbili.

TLR: * Msimulizi 1

M: Mara yangu ya kwanza kuenda kwenye onyesho la muziki ilikuwa siku yangu ya kuzaliwa. Bila kujua, rafiki zangu walininunulia tiketi na sikujua chochote hadi siku ilipofika. Nilipogundua kwamba wamenichukua kwenye ukumbi mkubwa wa muziki uliojaa taa, kelele na watu, nilifurahi sana. Nilivunjika moyo pale nilipogundua kwamba sikumjua mwimbaji hata mmoja aliyekuwa jukwaani kwa hivyo sikuweza kuimba chochote. Laiti ningalijua kuhusu onyesho hilo, ningalisikiliza nyimbo za waimbaji waliokuwa jukwaani na labda ningalikuwa shabiki wao. Hata hivyo, raha ya kuwa katika onyesho sitaisahau kamwe.

TLR: Msimulizi 2

- F:** Ninaposafiri, daima mimi hupenda kuenda kwenye maonyesho na matamasha ya muziki ili kujiunga na mashabiki wengine. Safari hii nilienda kwenye onyesho la muziki wa taarab na kwa kweli nilishangaa sana. Watu hawakupiga makofi baada ya nyimbo kupigwa bali walishika pesa mkononi na kutembea nayo huku wakicheza kwa mbwembwe mbele ya umati. Mwishoni, waliwatunza waimbaji kwa kuwapa hizo pesa. Nilihuzunika kidogo kwani sikuwa na pesa za kuwapa waimbaji. Ingawa nilifurahia kuvaa nguo nzuri, kujua nyimbo chache, lakini sina mpango wa kurudi pale tena.

TLR: Msimulizi 3

- M:** Safari hii nilipoenda kwenye onyesho la muziki wa taarab nilicheka sana nilipowaona watu waliokuwa wamekaa karibu na jukwaa huku wameshika makaratasi yaliyoandikwa maneno ya nyimbo zilizombwa na kuzisoma pale waimbaji walipoimba. Ingekuwa bora wangekariri maneno ya nyimbo walipokuwa makwao kwani walionekana kama washamba kweli. Nisingalitaka kuwa karibu nao asilani. Angalau walifahamu kuwa ni muhimu kuwatunza waimbaji pesa na si kukaa vitini kupiga makofi. Kwa kweli kila kitu huwa na utamaduni wake.

TLR: Msimulizi 4

- F:** Wiki iliyopita nilienda kwenye onyesho la muziki na rafiki zangu. Laiti ningalijua, ningaliwauliza rafiki zangu nguo ambazo zingefaa kuvaa. Kwa vile mimi nimezoea kuona maonyesho kwenye televisheni ambapo watu huonekana kuvalia sana, basi nilivaa nguo zangu nzuri zilizong'aa. Nilipofika huko nilijuta kwani watu walikuwa wamevaa nguo zao za kawaida kabisa. Uzuri ni kwamba tulikuwa mbali na jukwaa hivyo sikuhihi kama mimi ni mshamba. Lazima kusoma au kuulizia desturi za maonyesho kabla ya kuenda.

TLR: Msimulizi 5

- M:** Rafiki zangu walinichukua kwenye maonyesho ya muziki asilia wa huku Ulaya. Haikuruhusiwa kupiga makofi wakati nyimbo haijaisha, hata kama umeifurahia. Pia, nililazimika kukaa kimya, kutozungumza chochote wakati wote. Niliogopa hata kukohoa maana ningalitoa sauti ambayo ingekera hadhira ile. Ajabu ni kwamba, nilifurahia sana ukimya wa mashabiki kwa sababu niliweza kusikia vizuri. Pia, kwa bahati nzuri nilifahamu nyimbo nyingi pale kwani wazazi wangu walizipiga nilipokuwa mtoto.

TLR: Msimulizi 6

- F:** Kabla ya kupewa tiketi ya bure na rafiki zangu, niliamua kuwa nisingependa kuenda katika onyesho lolote la muziki. Nilipoenda nilipata kiti kizuri, mbele kabisa na niliweza kuwaona waimbaji kwa karibu sana ingawa kulikuwa na taa kali iliyochoma macho yangu. Nimewahi kuona kwenye televisheni jinsi watu wanavyovalia wakienda kwenye maonyesho nami nikavaa nguo yangu nzuri sana. Nilifurahi kwani watu wote walikuwa sawa na mimi. Sasa ninahisi nitajaribu kuenda kwenye maonyesho ya muziki angalau mara moja kwa mwezi. **

(Pause 5 seconds.)

TLR: Sasa sikiliza tena.

*(Repeat from * to **. Pause 30 seconds.)*

TLR: Huu ndiyo mwisho wa Zoezi 3. Baada ya muda mfupi utasikia Zoezi 4. Tumia muda huu kusoma maswali ya Zoezi 4.

(Pause 30 seconds.)

TLR: Zoezi 4

TLR: Utasikia mazungumzo kati ya mwandishi wa habari, Aaliyah akizungumza na Tom kuhusu maisha ya vijana katika jiji la Dar es Salaam.
Kwa kila swali chagua jibu sahihi kati ya A, B au C.
Weka alama ya tiki kwenye kisanduku sahihi.
Utasikia rekodi mara mbili.

F: * Tom, wewe ni mwanafunzi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, tuambie, ulianzaje huu mradi wa kuyaonyesha maisha ya vijana katika jiji la Dar es Salaam.

M: Niliona picha zilizobandikwa na vijana katika mitandao ya kijamii. Picha hizo zilionyesha shughuli tofauti za vijana katika miji yao. Wote walihusika na mradi ulioitwa 'kuwa na miaka ishirini jijini'. Kwa vile nina miaka 20 na ninapenda kubandika picha na video za jiji langu, nikaamua kuwaandikia wahusika kuuliza kama walishafikiria jiji langu. Walinijibu kuwa wangepurahi kuungana nami ili kulionyesha jiji la Dar.

F: Alaa. Halafu ukaanzaje?

M: Niliamua tangu mwanzo kwamba ninataka kuwaonyesha watu jiji langu huku mimi mwenyewe nikijifunza kuhusu mji wangu. Nilishauriwa kuenda maktabani kusoma makala kuhusu mji wangu. Lakini mimi nikaona ni bora kutembelea sehemu nilizozifahamu na kufanya utafiti wa kihistoria kwa kuongea na watu. Kwa mfano, nilienda Barabara ya Samora iliyo katikati ya mji ambapo kuna majumba mengi ya kihistoria na watu kutoka sehemu mbalimbali za jiji.

F: Ehee!

M: Nikaanza kwa kuzungumzia sanamu la askari lililopo katika barabara ya Samora. Katika utafiti wangu, niligundua kuwa sanamu lile ni kumbukumbu ya maaskari wa Kiafrika waliopigana vita vya kwanza vya dunia. Watu wengi hawajui kuwa waafrika walipigana katika vita hivyo; na hata pale pale sanamu lilipo, watu wengi walifikiri lile sanamu ni urembo tu au ni sanamu la kitamaduni kwa sababu limevaa kofia ya tarabushi, lakini si kweli.

F: Nimekuelewa. Baada ya kutembea pale unafanya nini?

M: Ninapakia picha, video na mazungumzo yangu na watu pale mjini katika tovuti maalumu. Wahusika wa mradi huu wanachagua picha zinazovutia zaidi halafu wanazibandika na kufahamisha umma kuwa ni mimi niliyewapelekea picha na video hizo. Nimegundua kuwa watu wengi wanavutiwa na picha ninazotuma na hunitafuta kuniuliza maswali zaidi.

F: Kama maswali gani?

M: Swali ambalo wengi huuliza daima ni kuhusu lugha inayozungumzwa na watu kwenye video ambayo ni Kiswahili. Wanataka kujua kama watu wote wanazungumza Kiswahili au wachache tu. Mimi huwajibu kuwa sisi huku tuna lugha nyingi ambazo tunazungumza. Kuna lugha za kikabila, Kiingereza, Sheng na Kiswahili chenyewe. Pia wachache huniuliza kama ninawalipa watu ninaowarekodi, na wengine huzungumzia nguo za watu waliorekodiwa.

F: Sasa wewe kama mwanafunzi wa chuo kikuu, unapata muda wa kusoma kweli?

M: Muhimu ni kujipanga tu! Kamwe siendi wakati wa shule, ingawa nimejitahidi siku za wiki baada ya kumaliza masomo kwani nimetaka kuwaonyesha watu jinsi jiji langu lilivyokuwa na kujaa foleni za magari. Ninapoamua kuenda kuzunguka, ninalazimika kubeba kila kitu kama maji ya kunywa na vitafunio ili nishitaji kununua vitu nikiwa nazunguka.

- F:** Lazima ni ghali sana kwako kuenda sehemu zote hizo, unafanyaje kuhusu pesa?
- M:** Huu mradi umenilipa pesa kidogo ili kunisaidia katika shughuli za kuonyesha mji wangu. Lakini kwa vile pesa yenyewe ni kidogo, mimi hutumia mabasi ya umma kama daladala au mabasi ya mwendo kasi. Usafiri ninaoupenda zaidi ni ule wa bajaji kwani ni salama zaidi na humfikisha mtu kwa haraka. Kama kuna foleni kubwa basi hupanda boda boda ambazo ni pikipiki zinazojichomeka kati ya magari na kuepuka foleni. Watu wengi wamevutiwa sana na aina tofauti za usafiri zilizopo hapa mjini.
- F:** Na huwa unasindikizwa na marafiki unapoenda kuzurura?
- M:** Mwanzoni nilitaka kuwachukua rafiki zangu ili tuende wote, lakini nimegundua kwamba ninapenda kufanya vitu mwenyewe. Ninapoenda peke yangu, ninajiamulia tu mwenyewe sehemu ya kwenda, ninaamua kama nina hamu ya kuzungumza na watu ninaokutana nao au la. Wakati mwingine ninachoshwa na majadiliano kuhusu mambo madogo madogo.
- F:** Kweli. Nimependa sana mradi wako! **

(Pause 30 seconds.)

TLR: Sasa sikiliza tena.

*(Repeat from * to **. Pause 30 seconds.)*

TLR: Huu ndiyo mwisho wa Zoezi 4, na mwisho wa mtihani.

Eng: This is the end of the examination.

Permission to reproduce items where third-party owned material protected by copyright is included has been sought and cleared where possible. Every reasonable effort has been made by the publisher (Cambridge University Press & Assessment) to trace copyright holders, but if any items requiring clearance have unwittingly been included, the publisher will be pleased to make amends at the earliest possible opportunity.

To avoid the issue of disclosure of answer-related information to candidates, all copyright acknowledgements are reproduced online in the Cambridge International Education Copyright Acknowledgements Booklet. This is produced for each series of examinations and is freely available to download at www.cambridgeinternational.org after the live examination series.

Cambridge International Education is the name of our awarding body and a part of Cambridge University Press & Assessment, which is a department of the University of Cambridge.